

Maswali

1. Nani alimchukia Samsoni?
2. Samsoni alimpenda nani?
3. Delila alitaka nini kwa Samsoni?
4. Wafilisti wangempa Delila fedha ngapi?
5. Taja kitu kimoja chenye Samsoni alisema kitamfanya awe dhaifu.
6. Ni nini hasa kingemfanya Samsoni awe dhaifu?
7. Nani alikata nywele za Samsoni?
8. Wafilisti walimfanya Samsoni nini?
9. Samsoni alifanya kazi gani gerezani?
10. Samsoni aliwauaje wafilisti?

Majibu

1. Wafilisti walimchukia Samsoni.
2. Samsoni alimpenda Delila.
3. Delila alitaka Samsoni amwambie nini itamfanya awe dhaifu.
4. Wafilisti wangempa kila mmoja vipande 1100 vya fedha.
5. Kamba mpya, miganda saba mbichi, fuma nywele yake.
6. Kukata nywele za samsoni ndiyo ingemfanya awe dhaifu.
7. Delila alikata nywele za Samsoni.
8. Wafilisti walitoa macho ya Samsoni.
9. Gerezani Samsoni alisaga ngano.
10. Samsoni aliwauwa Wafilisti kwa kuvuta na kuangusha hekalu lao

SHULE YA JUMAPILI YA CBM



Awamu ya 1 Mwaka wa 1

21 Samsoni na Delila

Marejeo

Waamuzi 16

Kiini cha somo

Kuonyesha Mungu mwishoe huwa na rehema(huruma) kila mara

Maneno maalum

1. Samsoni ana Mungu + nywele isikatwe + Wafilisti wanamchukia + Samsoni anapenda Delila + vipande 1100 vya fedha.
2. Nguvu + miganda 7 mbichi + Samsoni alifungwa + Samsoni aponyoka
3. Kamba mpya + Samsoni akata kamba.
4. Fumanisha nywele + Samsoni aponyoka tena
5. Nywele hazijakatwa + Samsoni dhaifu + macho yang'olewa na kufungwa + saga ngano.
6. Ombi kwa Mungu + Hekalu ikaanguka + Wafilisti wauawa

21.1 Waisraeli walipokuwa wamekaa kwa nchi ya ahadi, walianza kukufuru Mungu. Alituma taifa la nguvu liitwalo Wafilisti wawapige. Waisraeli walimlilia Mungu awasadie na akawatamia mtu wa nguvu aitwae Samsoni.

Mungu alimwambia Samsoni asikate nywele. Akitii Mungu ataendelea kuwa na nguvu.

Samsoni aliona mwanamke mfilisti na akampenda. Jina lake Delila. Wafilisti hawakumpenda Samsoni kwa sababu alikuwa na nguvu sana. Wafilisti walienda kuona Delila.

Wakamwambia, “Chunguza kwa nini Samsoni ana nguvu ili tumfungue. Halafu kila mmoja wetu atakupea fedha elfu na mia moja.”

21.2 Delila aliuliza Samsoni, “Tafadhali niambie ni nini inafanya wewe kuwa na nguvu nyingi na vile unaweza kufungwa.” Samsoni alisema, “Nikifungwa kwa miganda saba mbichi mpya nitakuwa dhaifu kama wanaume wengine.”



Wafilisti waliletea Delila miganda mbichi saba na akumfungia. Wafilisti walikuwa wamejificha ndani ya hiyo nyumba. Delila akasema, “Wafilisti ndio hawa.” Samsoni aliruka juu na kukata hizo kamba.

21.3 “Tafadhali niambie ukweli, nini inakufanya kuwa na nguvu?” Delila alimuuliza. Samsoni akamwambia, “Nikifungwa na kamba mpya zenye hazijawai kufanya kazi yoyote, nitakuwa dhaifu.”

Delila akamfunga na kamba mpya. Lakini Samsoni alizikata tena kama uzi.

21.4 Delila alilia akisema, “Umenidanganya.” Samsoni alimwambia, “Nitakuwa dhaifu ukizifumanisha hizi nywele zangu na ufunge kwa kigingi.” Akazifuma hizo nywele na kuzifunga, lakini Samsoni aliamka usingizini na kuzitoa kwa urahisi.

21.5 “Wawezaje kusema wanipenda?” Delila alilia, “Niambie nini inakufanya kuwa na nguvu?” Samsoni akamwambia Delila, “Sijawahi kukata nywele, nikikatwa nywele, nitakuwa dhaifu kama wanaume wote.”



Samsoni alipokuwa analala, Delila alimkata nywele. Delila akamwambia, “Samsoni Wafilisti wako hapa.”

Samsoni aliamka dhaifu akijua nguvu zimemuondoka. Hakuwa nayo tena, Wafilisti wakamshika na kumfunga. Walimchukuwa samsoni na kumtoa macho, akawa kipofu. Wakamweka gerezani na kumfanya asage ngano kila siku.

21.6 Wakati moja Wafilisti walikuwa na karamu kubwa juu ya paa ya hekalu wakamleta. Samsoni kutoka gerezani na kumcheka.

Samsoni aliomba, “Ee Bwana Mungu nipe nguvu mara hii tu, nilipize kisasi kwa Wafilisti.”

Samsoni na nguvu zake zote alishika na kuvuta nguzo za hekalu. Hekalu ilianguka kwa kishindo na Samsoni akafa pamoja na Wafilisti wote.

